# Tani milioni tano za nyama zawanufaisha wafugaji

Singida
**CLAUDIA KAYOMBO**

ZAIDI ya tani milioni 5.4 za nyama yenye thamani ya zaidi ya sh. bilioni 40.89 zimezalishwa kwa kipindi cha miaka miwili mkoani hapa na kuwanufaisha wafugaji.

Mkuu wa Mkoa Singida, Peter Serukamba, aliyasema hayo wakati akielezea mafanikio yaliyofikiwa na mkoa katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Alisema majosho manne yenye thamani ya sh. milioni 144 yamejengwa katika kipindi hicho huku mengine 26 yenye thamani ya sh. milioni 598 yanamaliziwa ujenzi wake katika kipindi cha mwaka huu.

"Kuongezeka kwa upatikanaji wa dawa za ruzuku na uogeshaji mifugo mkoani, lita 2,458 za dawa zenye thamani ya sh. milioni 110.6 zimepatikana katika kipindi cha miaka miwili," alisema.

Alifafanua kuwa hatua hiyo imesababisha magonjwa ya mifugo yasababishwayo na kupe, inzi na mbu kupungua huku zaidi sh. bilioni 9.46 zimetumika kwa shughuli za kilimo ambapo tani 1,565.8 za mbolea ya ruzuku zilinunuliwa kwa zaidi ya sh. bilioni4.3 kisha kusambazwa kwa wanufaika 8,342.

"Tani 856.48 za mbegu za alizeti zenye thamani ya zaidi ya sh. bilioni 3.9 zilipokelewa na kutumika kwa wakulima katika msimu wa mwaka 2021/2022 na 2022/2023," alisema Serukamba.

Vilevile, alisema sh. milioni198 zimetumika kwa ajili ya kununulia pikipiki 66 za ofisa ugani wote ndani ya mkoa wa Singida ili kuongeza utoaji wa huduma za ugani.

Scanned with CamScanner
CamScanner